OPEN ACCESS
Int. J. Educ. Found. 03 (03) 2026. 565-572 DOI: 10.33687/ijef.003.03.00142
Check for updates
IJEF
Available Online at EScience Press
International Journal of Education Foundations
ISSN: 3078-7866 (Online), 3078-7858 (Print)
https://ijef.esciencepress.net

RESEARCH ARTICLE

# Mwingiliano wa Ufundishaji, Lugha ya Kiswahili na Mazingira ya Ujifunzaji katika Kujenga Umahiri wa Lugha na Maarifa kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi nchini Tanzania

**Steven Yesaya**
*Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Tanzania*

**Corresponding Author**
*Steven Yesaya, Email: steveyesaya1@saut.ac.tz*

**_Author's Contributions_**
*All authors contributed equally to this research.*

**_Article History_**
*Received February 27, 2026; Accepted: April 13, 2026; Published: July 24, 2026.*

## IKISIRI

Makala hii inachunguza nafasi ya mwingiliano wa ufundishaji, matumizi ya lugha ya Kiswahili na mazingira ya ujifunzaji katika kujenga umahiri wa lugha na maarifa kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini Tanzania. Lengo kuu la makala ni kubainisha namna lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia inavyoathiri uelewa wa wanafunzi katika masomo mbalimbali pamoja na ushiriki wao katika mchakato wa ujifunzaji darasani. Utafiti wa Makala hii umeongozwa na nadharia ya Ujenzi wa Maarifa ya Lev Vygotsky, inayosisitiza kuwa lugha ni nyenzo muhimu ya kujenga fikra, maarifa na kukuza ujifunzaji wa mwanafunzi kupitia mwingiliano wa kijamii. Mbinu za utafiti zilizotumika ni uchambuzi wa nyaraka, mahojiano, pamoja na uchunguzi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji huchochea uelewa wa dhana za kitaaluma kwa wanafunzi wa shule za msingi, huimarisha ushiriki wa wanafunzi darasani na kukuza uwezo wa kufikiri kwa kina. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa bado kuna changamoto zinazohusiana na uhaba wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia pamoja na mitazamo hasi ya kijamii kuhusu nafasi ya Kiswahili kama lugha ya maarifa. Makala inapendekeza kuimarishwa kwa sera ya lugha ya kufundishia, kuendelezwa kwa istilahi za kitaaluma za Kiswahili, pamoja na kuboreshwa kwa mazingira ya ujifunzaji ili kuongeza ufanisi wa elimu ya msingi nchini Tanzania. Utafiti unahitimisha kuwa Kiswahili kina nafasi muhimu katika kujenga msingi wa umahiri wa lugha na maarifa kwa wanafunzi na hivyo kuchangia kuboresha ubora wa elimu nchini.

**Keywords:** Kiswahili; lugha ya kufundishia; mazingira ya ujifunzaji; umahiri wa lugha; maarifa; elimu ya msingi; Tanzania

## UTANGULIZI

Makala inaanza kwa kufungua mjadala ufundishaji na ujifunzaji katika muktadha wa elimu kwa kutumia Kiswahili. Utafiti uliofanywa na Onyango (1990) nchini Kenya ulionesha wazi kuwa wasomi wengi walikuwa na mtazamo hasi juu ya matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji na shughuli nyingine za kila siku. Kwa ujumla, katika taaluma ya elimu, dhana ya ufundishaji si dhana mpya kwa wadau mbalimbali ikihusisha wanafunzi, walimu na wazazi. Suala la ufundishaji lugha lilianza kutiliwa mkazo katika nchi za Kimagharibi mapema katika karne ya 14 wakati Kilatini kilipokuwa lugha peke ya matumizi katika shughuli za kibiashara, elimu, dini na utawala. Hivyo, ufundishaji hurejelea mchakato wa makusudi unaofanywa na mwalimu ili kuwezesha upatikanaji wa maarifa, stadi na mitazamo kwa mwanafunzi, ilhali ujifunzaji ni matokeo ya mchakato huo unaojidhihirisha kwa mabadiliko ya kitabia, kiakili au kimtazamo kwa mwanafunzi. Hata hivyo, katika karne ya 16 lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kiitaliano zilianza kutambuliwa kwa sababu ya mabadiliko ya kisiasa (Richard na Rodger, 1986).

Katika mfumo wa elimu nchini Tanzania, Kiswahili kimeteuliwa kuwa lugha kuu ya kufundishia katika ngazi ya elimu ya msingi kwa masomo yote isipokuwa somo la Kiingereza na kuwa ndiyo lugha ya mawasiliano. Lugha mawasiliano ni lugha itumikayo kwa ajili ya mawasiliano kati ya watu wenye lugha zaidi ya moja (Massamba, 2016). Hali hii inaifanya lugha hii ya Kiswahili kuwa nyenzo muhimu katika kufanikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, kwa mantiki hiyo, lugha ndiyo chombo kikuu cha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Mwanafunzi hupelekwa shuleni kwa lengo la kupata maarifa na ujuzi mpya, huku jukumu la mwalimu likiwa ni kuratibu na kuongoza mchakato huo wa kujifunza kwa ufanisi zaidi.

Nchini Tanzania mnamo mwaka 1967 utakumbukwa katika historia ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha lililofafanua siasa ya ujamaa na kujitegemea. Katika kufanikisha elimu ya kujitegemea, suala la lugha lilihitaji kushughughulikiwa na kuwekwa wazi; Sewangi (2004). Katika kipindi hicho Baraza la Kiswahili Taifa (BAKITA) lilianzishwa. Kufikia mwaka 1968 Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya kufundishia elimu ya msingi katika masomo yote isipokuwa somo la Kiingereza. Kabla ya hapo Kiswahili kilitumika katika madarasa manne tu ya mwanzo katika shule za msingi huku Kiingereza kikitumika katika madarasa yote ya juu. Msanjila (1990) anaongeza kuwa kwa uamuzi mwingine uliofanyika baadae ni kuifanya lugha ya Kiswahili kutumika katika kufundishia vyuo vya ualimu wa shule za msingi.

Aidha, ufundishaji na ujifunzaji ni dhana zinazotegemeana na zinazokwenda sambamba, ambapo uwepo wa mmoja huchochea uwepo wa mwingine. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa suala la ujifunzaji linaweza pia kutokea nje ya mazingira rasmi ya darasani bila uwepo wa mwalimu. Katika hali hiyo, mazingira yenyewe huchukua nafasi muhimu kama kichocheo cha ujifunzaji, kwa kuwa mwanafunzi anaweza kupata maarifa na uzoefu kupitia mwingiliano na mazingira halisi yanayomzunguka.

Kwa msingi huu, utangulizi huu unaweka bayana muktadha wa kuchunguza kwa kina nafasi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika kuimarisha ujifunzaji na kujenga umahiri wa lugha pamoja na maarifa kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini Tanzania.

## DHANA YA UFUNDISHAJI

Dhana ya ufundishaji imepewa tafsiri nyingi na wataalamu wa elimu, lakini kwa ujumla hurejelea mchakato wa makusudi unaofanywa na mwalimu ili kuwezesha ujifunzaji kwa mwanafunzi. Kwa mujibu wa Bruner (1960), ufundishaji ni juhudi ya kimfumo inayolenga kumwezesha mwanafunzi kujenga maarifa mapya kwa kuhusianisha yale anayoyafahamu tayari na uzoefu mpya. Mtazamo huu unaonesha kuwa ufundishaji si utoaji wa taarifa pekee, bali ni mchakato wa kuwezesha ujengaji wa maarifa. Utoaji na upataji wa maarifa uhusisha matumizi ya lugha kama mhimili mkuu wa mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi.

Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu (1984) ilielekeza kuwa, Kiswahili kitumike katika nyaja za kijamii na kisiasa, elimu ya msingi, vyuo vya ualimu wa shule ya msingi na elimu ya watu wazima. Huku, lugha ya Kiingereza ikipangiwa kutumika maeneo ya sekondari, elimu ya juu mahakama zote isipokuwa ya mahakama za mwanzo, nyanja za sayansi na teknolojia na diplomasia ya kimataifa. Kutofautisha huku ulipingwa vikali na baadhi ya wataalamu kama vile Mulokozi (1989) kuwa ulilenga kuitukuza lugha ya Kiingereza na kushusha hadhi ya lugha ya Kiswahili.

Katika kupata maoni kuhusu dhana ya ufundishaji, uchunguzi huu uliweza kufanya mahojiano na waalimu kutoka shule za msingi teule zinazopatikana katika Wilaya ya Mbozi Mkoani Songwe. Katika kuanza na mjadala huu, Makala haya yametumia misimbo yenye herufi kuwakilisha majina ya shule husika; na yafuatayo ni maoni ya walimu kutoka shule za msingi XY, BB na MN ambao kwa maoni yao waliweza kuifasili dhana ya ufundishaji. Kutokana na maana hizo na makala hii imeweza kudondoa maoni hayo kwa ufupi kama walivyosema huku misimbo ya herufi A, B, C na D kuwasilisha majina ya waalimu hao:

- Mwalimu A alisema: Ufundishaji ni kitendo cha kutoa maarifa na elimu fulani kwa wanafunzi katika ngazi husika.
- Mwalimu B alisema: Ufundishaji ni uwezeshaji wa taaluma aliyoipata mwalimu kwa wanafunzi darasani au nje ya darasa.
- Mwalimu C alisema: Ufundishaji ni kitendo cha uhawilishaji wa maarifa fulani kutoka kwa mwalimu kwenda kwa wanafunzi
- Mwalimu D alisema: Ufundishaji ni mchakato wa kufunza jambo, dhana, tukio, hali kwa wanafunzi katika ngazi na viwango mbalimbali.

Dhana hizi kuhusu ufundishaji zimeweza kutusukuma kujadili dhana ya ufundishaji kwa ujumla kutokana na mielekeo ya walimu katika kuifasili dhana ya ufundishaji. Garder (1985) anasema mielekeo inaelekezewa kitu au jambo fulani; na imani ya mtu kuhusu kitu au jambo fulani ndiyo msingi wa mielekeo

yake. Mwelekeo wa maana kutoka kwa mwalimu A, unasisitiza ufundishaji ni kitendo cha kutoa maarifa na elimu kwa ngazi husika. Makala hii imeona maana hii kuwa na mapungufu yake, kwani inasisitiza ufundishaji kuzingatia ngazi. Ufafanuzi huu unatokana na mambo makuu mawili, kwanza dhana yenyewe kufafanuliwa kijumla jumla. Pili ufafanuzi unaotolewa na kuacha baadhi ya misingi muhimu katika kazi ya ufundishaji. Katika sababu ya kwanza ya ujumla katika dhana hizo ni maneno yanayotumika kufafanua dhana ya ufundishaji kama; utoaji wa elimu, maarifa na uwezeshaji wa taaluma.

Neno ufundishaji (n) (teaching) linatokana na funda, funza au fundisha (vt) (teach), lenye maana ya kusaidia mtu kujifunza jambo fulani kwa kumpa maelekezo. Encyclopaedia Britanica (EB) juzuu 18, wanasema kwamba, ufundishaji ni dhana ya muda mrefu. Dhana hii inalinganishwa na kipindi cha mwanadamu kuwepo katika uso wa dunia. Aidha, ufundishaji unatazamwa kama dhana inayotanguliwa na dhana mwenza, yaani ujifunzaji na dhana hizi haziwezi kutenganishwa kwa namna yoyote (Madila na Yesaya, 2025). Ufundishaji katika jamii za mwanzo, ambazo hazikuitambua dhana hii kama inayoendana na kuwepo kwa taasisi (shule na vyuo) zinazoisimamia, ilifasiliwa kama maelekezo au uzoefu wa mpangilio wa jambo, hali na kitu kimoja dhidi ya kingine. Dhana hii ilijikita katika kuyatalii na kuyabainisha mazingira katika hali na mabadiliko mbalimbali yaliyojitokeza. Pia, ilikuwa katika kujaribisha kila kilichokuwa katika mazingira hayo ili kugundua manufaa ya kila kilichokuwa katika mazingira husika na kwanini kipo mahali kilipo wakati huo.

Kabla ya mifumo na taasisi za ufundishji na ujifunzaji kama vile vituo vya watoto, shule na vyuo kuanzishwa, ufundishaji na ujifunzaji lilikuwa jukumu la wazazi, wazee na makasisi (wazee wa kimila). Wanajamii hawa waliwafundisha watoto wao na vijana maarifa mbalimbali yaliyoelekeana na mahitaji ya mazingira yao. Mwanadamu alikubalika katika jamii kwa kuwa na uwezo wa kufundisha wenzake. Akinukuliwa Aristotle katika Ensyclopaedia Britanica juzuu na; 18 anasema;

> Alama ya hekima na busara kwa mwanadamu ni uwezo wake katika kufundisha kile anachokijua au alicho na uzoefu nacho. Kujua, kufanya, kufundisha na kujifunza ni masuala yaliyoanza karne nyingi na hata leo ni vigumu kuyatenganisha katika jamii zetu.

Maelezo haya yatuelekeza kwamba, suala la kuitaka au kuona jamii ikipata maarifa juu ya mambo yenye tija kwa maisha ya watu wanaounda jamii husika lilikuwa jukumu la kila mwanajamii. Hii ilitokana na kwamba kila mwanajamii alitakiwa kuhakikisha vijana wanapatiwa uwezo wa kutenda, kuhisi, kufikiri na kuamini juu ya maisha endelevu ya jamii zao. Ufundishaji wa aina hii haukufuata utaratibu wa kitaasisi kama ilivyo leo; mchakato mzima ulifuata taratibu za kiutawala ambazo pia hazikuwa rasmi. Watu waliokuwa na uzoefu katika masuala mbalimbali ya kijamii na kimazingira walifanya kazi hii.

Maelezo yanayotolewa hapo juu yanatuacha na swali la msingi. Je, ni mbinu gani na maudhui yapi yalifundishwa? Swali hili linatoa mwanga kuelekea kuelewa dhana nzima ya kufundisha. Kabla ya mifumo rasmi ya kitasisi, elimu iliyotolewa iliangalia mazingira halisi na maisha jamii iliyoishi. Kwa mfano, kama jamii iliyohusika ilikuwa ikijishughulisha na kilimo au uganga, au uhunzi pamoja na mazingira husika kijiografia maudhui ya kilichofundishwa yalilazimika kufuata mkondo huo. Hii ni kusema kwamba vijana walifundishwa namna ya kutumia mazingira waliyoishi kuendeleza maisha yao na kuepuka mambo ambayo yangesababisha hatari katika maeneo yao na jamii zao kwa ujumla. Vijana walifundishwa tabia njema, sheria na taratibu, historia za jamii zao hususani mashujaa, viongozi na watu waliotokea kutenda mambo ya kukumbukwa katika jamii hizo, nyimbo na masimulizi ya jamii zilizotangulia, mila na desturi za jamii, miiko na mengine. Haya hayakutokea katika vipindi fulani, bali yalikuwa ni matendo yaliyofanyika katika taratibu halisi za maisha waliyoishi wanajamii husika.

Mbinu zilizotumika kufundisha zilikua ni rasmi na zisizorasmi. Kwa upande wa mbinu zisizorasmi, vijana walifundishwa mambo mbalimbali kupitia michezo ya kuigiza, kuigiza shughuli kadhaa zilizofanywa na wazee, hadithi na masimulizi, visakale na visasili, nahau na methali, matendo mbalimbali na nyimbo. Vijana walijengewa moyo wa uoga ili kuogopa kutenda matendo ambayo hayakukubalika katika jamii. Aidha, shughuli za mikono zilitumika kufundishia baadhi ya masuala yaliyohusu utendaji.

Katika mfumo rasmi, ufundishaji ulijumuisha nadharia na vitendo ambavyo vililenga kuwajengea vijana maarifa na ujuzi wa kukabiliana na maisha halisi katika mazingira yao. Aidha, mbinu hizi zilitumika moja kwa moja katika kazi halisi kama za kilimo, ufugaji, uhunzi, uchongaji, ufinyanzi, au uwindaji kutegemea shughuli zilizokuwa katika mazingira husika. Maelekezo mengine yalitolewa kinadharia na wazee au watu maalum katika jamii hizo. Mafunzo ya namna hii yalijumuisha masuala yaliyoelekeana na mila na

tamaduni za jadi, taratibu na sheria, kusahihisha na kupewa mitazamo ya namna walivyoweza kuzilinda na kuzitunza jamii zao. Mwanafunzi alihesabiwa kama amejifunza kulingana na jinsi alivyowezakumudu maisha yake na jamii iliyomzunguka.

Dhana ya ufundishaji na ujifunzaji ilikuja kuwa maarufu katika karne ya 18 baada ya mageuzi ya viwanda Ulaya. Ufundishaji na ujifunzaji ndipo ulipotolewa katika jamii na kupelekwa katika taasisi maalum za shule na vyuo.

**Kuelekea Ufundishaji**

Kabla ya kujishughulisha na lolote jambo la kwanza ni kujiuliza maswali yafuatayo;

i. Kufundisha ni nini?
ii. Unamfundisha nani?
iii. Unafundisha nini?
iv. Baada ya ufundishaji unataka nini katika aliyefundishwa?

Haya ni maswali ya jumla ambayo yakizingatiwa vema yatamfikisha mwalimu katika malengo yake ndani na nje ya darasa. Tukianza na swali la kwanza, hapo juu tunasema kwamba kufundisha ni kuwezesha mwanafunzi au mjifunzaji kupata maarifa juu ya jambo, tukio, hali au suala fulani. Maarifa kwa mujibu wa Mwanahewa, (1997) ni kumbumbu ya hali halisi katika mazingira husika. Mwanahewa (keshatajwa) anabainisha kuwa kufundisha ni mchakato wa kupanga na kuwasilisha maarifa kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kumwezesha mwanafunzi kujifunza kwa urahisi. Aidha, hali halisi hujumuisha uzoefu, mielekeo, na tabia anayoipata mwanafunzi. Kwa mwelekeo huu tunaweza kung'amua kama kumbukumbu ya mwanadamu inao uwezo wa kupata maarifa yanayotarajiwa au la.

Wanadamu wameumbwa tofauti, ingawa wote wana mifumo inayofanana. Hali hii huwafanya kuwa na mahitaji yanayotofautiana. Kwa mfano, kama ukiwachukua watoto nje ya darasa ukawaweka kwenye mstari kutoka eneo moja na kuwaamlisha kukimbia kutoka sehemu hiyo mpaka sehemu nyingine tunajua kwamba hawawezi kufika sehemu ya kumalizia pamoja. Kwa namna yoyote kutakuwa na tofauti kati ya mtoto wa kwanza, pili mpaka wa mwisho. Na hata ukiwapa chakula kinacholingana kwenye sahani na kuamlisha kuanza kula kwa wakati mmoja, bado kutakuwa na mtoto atakayeanza kumaliza na atakaye maliza mwishoni. Zoezi hilo unaweza kulirudia kwa mara nyingi na katika vitu tofauti na utagundua kwamba hawawezi kufanya matendo hayo katika viwango vinavyolingana.

Walimu wengi walioko madarasani na wale wanaotarajiwa wanadhani kwamba darasa lenye watoto wengi wanaweza kujifunza kwa viwango na kasi inayolingana. Kama matendo ya kawaida hawawezi kuyafanya kwa viwango na kasi inayolingana inawezekanaje wanafunzi hao wajifunze kwa kiwango na kasi inayolingana? Fikra ya kudhani wanafunzi wanauwezo wa kujifunza kwa viwango na kasi inayolingana ni mitazamo ya kudhani tu. Maswali hapo juu yanamweka mwalimu katika daraja la juu zaidi na kuona mwanafunzi kama mpokeaji tu. Mtazamo huu hujumuisha viwango vya kumbukumbu kwa watu waliozaliwa, kulelewa na kukulia katika mazingira tofauti. Mtazamo huu unamadhara makubwa kwa watoto, wazazi, na taifa linalohusika. Kwa mfano, katika shule XY mwalimu wa somo la Kiswahili aliingia darasani kufundisha taratibu za uundaji wa maneno kwa wanafunzi wa darasa la tano. Kwa kuwa mwalimu aliandaa somo lake vizuri na kutoa maelekezo kwa uangalifu na kutumia zana sahihi alidhani amefanikiwa kwa asilimia zote. Baada ya kumaliza kufundisha somo lake, alipouliza maswali kuhusiana na mada hiyo alishikwa na mshangao kuona baadhi ya wanafunzi wamekosa majibu ya maswali yake ya uundaji wa maneno. Mwalimu akadhani kuwa hao wanafunzi hawakumsikiliza wakati wa ufundishaji au ni wajinga. Je mwalimu huyu alikuwa sahihi?

Katika nchi zinazoendelea, utafiti unaonesha kwamba darasani kuna wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa kushika kilichofundishwa haraka hata kabla ya mwalimu kukamilisha ufafanuzi wa kile anachokifundisha. Kielelezo kifuatacho ni data kutoka katika darasa lenye wanafunzi 53 wa darasa la tano kutoka shule moja kati ya shule tatu kutoka wilaya ya Mbozi.

Katika jedwali Na.1 hapo juu, data zinaonesha kuwa kati ya wanafunzi 53 wa darasa la tano katika shule XY, wanafunzi 14 sawa na asilimia 26.4 walikuwa katika kiwango cha juu cha ujifunzaji. Wanafunzi hawa walionesha uwezo mzuri wa kuelewa maelekezo ya mwalimu, kujibu maswali kwa usahihi na kushiriki kikamilifu katika kazi za darasani na kufanya vema maswali waliyokuwa wamepewa na mwalimu. Wanafunzi 25 sawa na asilimia 47.2 walikuwa katika kiwango cha wastani. Kundi hili liliweza kuelewa maudhui ya somo kwa mwongozo wa kawaida wa mwalimu, ingawa baadhi yao walihitaji maelezo ya ziada katika maeneo fulani. Aidha, wanafunzi 14 sawa na asilimia 26.4 walikuwa katika kiwango cha chini cha ujifunzaji. Wanafunzi hawa walihitaji ufuatiliaji wa karibu, mifano zaidi na mbinu shirikishi ili kuwawezesha

kuelewa vizuri zaidi maudhui ya somo. Matokeo haya yanaonesha kuwa utofauti wa ujifunzaji darasani upo kwa kiwango kinachohitaji mwalimu kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji ili kukidhi mahitaji ya kila mwanafunzi.

Jedwali Na. 1. Mgawanyo wa wanafunzi kwa kuzingatia utofauti wa ujifunzaji

| Daraja la utofauti wa ujifunzaji | Maelezo ya wanafunzi | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Kiwango cha juu | Wanafunzi wenye kuelewa haraka, hushiriki kikamilifu na kufanya kazi kwa usahihi mkubwa | 14 | 26.4% |
| Kiwango cha wastani | Wanafunzi wanaoelewa kwa mwongozo wa kawaida na hushiriki kwa kiwango cha kati | 25 | 47.2% |
| Kiwango cha chini | Wanafunzi wanaohitaji msaada wa karibu wa mwalimu na muda zaidi wa kujifunza | 14 | 26.4% |
| Jumla | | 53 | 100% |

Hata hivyo, sababu kubwa za mgawanyo huu zipo dhahiri katika jamii zetu. Moja ni mazingira halisi ya mtoto tangu akiwa tumboni, wakati wa kuzaliwa, baada ya kuzaliwa, na jamii inayomzunguka anapoanza kutangusana na wanajamii wanaomzunguka. Pili, ni mgawanyo wa rasilimali. Jamii nyingi za Kitanzania na nchi zinazoendelea zinakubaliana kwamba mgawanyo wa rasilimali hauko sawa katika jamii moja na nyingine. Suala la mgawanyo wa rasilimali linaweza kuchukua nafasi kubwa sana katika kumwandaa mtoto katika kuwa na uwezo na kasi ya kujifunza inayotakiwa. Masuala haya yanategemeana kwa kiasi kikubwa katika kuleta athari chanya au hasi kulingana na hali halisi za maisha. Aidha, mgawanyo wa rasilimali ndio unaoamua mazingira ya mtoto katika jamii zetu. Ni jambo lililozoeleka katika jamii nyingi za Kitanzania kukutana na jamii mbalimbali kushindwa kupata japo mlo mmoja. Hata kama mlo huu ukipatikana uwezekano wa kupata utakaofuata unategemea majaliwa ya Mwenyezi Mungu.

Jamii ni tasisi yenye uwezo wa kuandaa mtoto katika kuyakabili maisha yake kiimani, kiutamaduni na kitaaluma. Yapo mambo ya msingi ambayo humfanya mtoto kukua vizuri au vibaya kitaaluma yanayopatika katika jamii zinazomzunguka mwanafunzi. Kwanza kabisa ni taratibu za maisha kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Sababu hii inaendana na sababu nyingine ya mazingira halisi ya shule. Mazingira bora yana mchango mkubwa katika kumfanya mwanafunzi kuongeza bidii ya ujifunzaji na kinyume chake. Turejee picha ya jengo la madarasa ya wanafunzi kiwakilishi.

Kwa kulinganisha kielelezo hapo juu na mazingira halisi ya mwanafunzi anayesoma katika shule hiyo, unapata picha gani? bidii yake, uwezo wake, kasi yake katika kujifunza itakuwaje? Je, ushindani wake na wanafunzi wanaosoma katika shule zenye mazingira rafiki katika viwango vya ujifunzaji utakuwaje? Hali za majumbani kwa wanafunzi wanaosoma mazingira hayo zipoje?



**Mchoro 1.** Moja ya madarasa katika shule za Wilaya ya Mbozi

Maswali yanayotangulia yanakufikisha katika kuona tofauti zinazojitokeza baina ya mwanafunzi mmoja na mwingine yakiwa ni matokeo ya mazingira. Shule na madarasa yake siku zote yanamulika hali halisi ya jamii zinazoizunguka. Hii ni kutokana na kwamba shule kama taasisi ni mali ya jamii katika maeneo husika. Chombo hiki huonesha hali ya uchumi, siasa na utamaduni wa wanajamii. Jamii inayojivunia elimu kama chombo cha ukombozi kiuchumi na kisiasa haiwezi kufumbia macho chombo hicho kikiwa katika mazingira mabaya yasiyo na tija katika jamii hiyo. Na mifumo ya kisiasa inapoona jamii ikiwa na mwamko katika jamii hufanya kadri inavyowezekana kuweka miundo mbinu inayokubalika katika jamii. Pamoja na uchumi mbaya katika jamii nyingi za kitanzania hali ya mazingira inachangia kuendelea kudidimiza ndoto na matarajio ya walio wengi kuelekea ustawi wa jamii zao.

Hii ni kutokana na wanajamii walio wengi kuonekana kukata tamaa na kuona kwamba mifumo ya kisiasa haina la kufanya kuhakikisha maendeleo ya jamii zake yanapiga hatua.

**MAZINGIRA YA MWANAFUNZI NA MATOKEO YA UJIFUNZAJI**

Mwanafunzi kwa maana ya mtoto hujifunza kutoka kwa watoto wenzake, wazazi wake, wanafamilia, wanajamii, shuleni, na kwa kuchunguza mambo mbalimbali yanayomzunguka. Hivi ni vigezo vya kimazingira ambavyo huwa na matokeo makubwa katika kumjenga mtoto kimwili, kiakili, matarajio yake ya baadae, mahusiano, kitabia, kihaiba, uwezo wa kutambua na kuchanganua na mielekeo yake kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Mataifa yanayotazama elimu na tasisi zake kama msingi wa maisha bora ya jamii zake huimarisha viashiria vya kimazingira na kuvifanya kuwa rafiki kwa watoto wao. Rejea kielelezo hapo juu kama mfano katika eneo hili. Ni ukweli usio na shaka kwamba, ukiingia ndani utakutana na vumbi, hakuna madawati, na mambo mengine. Aidha, utafiti uliofanyika unaonesha hali mbaya zaidi katika maeneo mbalimbali ya nchi. Hii ni kuonesha kwamba kiwango cha ujifunzaji kwa wanafunzi wanaokurubiana na mazingira ya namna hiyo kitakuwa duni na hata maisha yao kwa ujumla. Kujifunza ni kugeza na kuzoea hali, matendo na tabia mbalimbali. Mtoto anayejifunza huiga mambo mengi katika jamii inayomzunguka. Uigaji huu waweza kuwa hasi au chanya kutegemea mhusika anachokiiga. Jamii zenye wanajamii wa kupigiwa mfano, hujikuta mara zote watoto na vijana wakiwaiga matendo, tabia na hata mienendo yao. Katika kujifunza watoto wengi hutamani kuwa watu fulani kutoka jamii zao kulingana na jinsi walivyo mifano ya kuigwa. Kinyume chake katika jamii ambazo hazina mwanga kielimu watoto watawaiga watu gani? Wakulima au wafugaji tena wasio na mbinu bora za shughuli zao, kwa kuwa ndio waliopo katika jamii hizo? Jamii ya aina hii inategemewa kuwaje baadae? Taifa nalo litakuwaje baadae? Haya ni maswali yanayotufikisha katika kuamini kwamba taifa lililojigawanya kitaaluma na kielimu litajenga matabaka ya watawala na kati ya watu wenye uwezo kielimu na kimaamuzi.

Mwalimu kutambua kwamba wateja wake ambao ni wanafunzi alionao darasani wanatofautiana katika uwezo wa kujifunza ni hatua moja na ya msingi. Hatua inayofuata ni kwamba, anatakiwa kuhakikisha ujifunzaji umetokea kwa wanafunzi wake. Ukirejea dhana ya ufundishaji kwamba ni mchakato wa kuwezesha ujifunzaji wa maarifa mapya, utaona kwamba kama ujifunzaji haujatokea upande wa pili, bado ufundishaji hautakuwa na maana yoyote. Kwa mfano, kama mwalimu wa lugha anafundisha namna ya kuandika irabu ‘a’ kwa wanafunzi wa awali, mpaka mwisho wanafunzi wake wakashindwa kuandika hiyo irabu, mwalimu huyo atasema kwamba amefundisha? Au mwalimu amemaliza kufundisha mada ya ‘aina za maneno’ na wanafunzi wake wakashindwa kubainisha aina za maneno katika sentensi, ufundishaji huu utachukuliwaje? Kwa ujumla hakutakuwa na maelezo yanayotosheleza kuthibitisha ufundishaji endapo upande wa pili haukujifunza.

Mwalimu anapoingia darasani iwe katika somo la lugha au aina nyingine ya somo, anatakiwa kuhakikisha ujifunzaji umetokea. Walimu wengi wanajielekeza sana katika chaki ubaoni na maneno mengi katika kuelezea wanachokifundisha. Wengi wetu tunadhani hiyo ndiyo mbinu bora ya kufundisha, tunakuwa sawa na madaktari kutoa dozi kwa mgonjwa ili apone. Wanafunzi si wagonjwa kama tunavyodhani. Mwisho wa kazi zetu tunakuta ule ugonjwa tuliokuwa tunautibu hauponi. Kumbe tulikosea kwa kujivisha majukumu yasiyokuwa yetu.

Ujifunzaji ni uigaji, urudiajirudiaji wa matendo yanayotakiwa kujifunza. Chukua mfano, wa fundi selemela akimfundisha mwanafunzi njia za kutengeneza meza au kabati mwanafunzi wake kwa kumpa maelezo bila kutenda. Baada ya maelekezo hayo, ampe mwanafunzi huyo vifaa vya kutengenezea kabati au meza. Je, mwanafunzi huyo ataweza kulitengeneza hilo kabati au meza? Je, njia pekee za kutengeneza meza au kabati zitamsaidia kumudu hata matumizi ya vifaa vya uselemala? Jibu utakalolitoa litakuwa hapana.

Maelezo hayo hapo juu yanatukumbusha kwamba, mwalimu unapoandaa somo lako lazima ujiulize ‘Nini natakiwa wanafunzi wangu wafanye darasani? Hii ni kutokana na kuwa, kama wewe mwalimu utaandaa somo ambalo wewe ni msemaji tangu mwanzo mpaka mwisho, hapa na pale ukiuliza maswali mwishoni mwa kipindi kama tulivyozoea, basi ujifunzaji unaokusudiwa hautafikiwa.

Walimu mara nyingi hujisikia hasira wanafunzi wanaposhindwa kujibu maswali ya kilichofundishwa au wanafunzi wanapopoteza usikivu darasani. Tunashindwa kujiuliza kwanini imetokea kama ilivyotokea. Je, kosa na sababu ya kukosa usikivu kwa wanafunzi wangu ni langu (mwalimu), au linatokana na mazingira? Au hali ya wanafunzi? Maswali haya

yanakusaidia mwalimu kutatua tatizo kabla halijawa kubwa kupindukia. Ikigundulika kosa linatokana na wewe mwalimu rekebisha haraka inavyowezekana na kama ni wanafunzi wenyewe tafuta njia za kulitatua haraka pia. Matatizo ya wanafunzi yanaweza kutokana na mazingira halisi ya darasani, shuleni, au hata nyumbani wanakotoka. Yale ya nyumbani kwao, unashauriwa kuonana na wazazi ili kuwaelimisha juu ya matatizo ya watoto wao na yale ya shuleni uongozi wa shule na serikali waelezwe juu ya changamoto ili kutafuta ufumbuzi. Hii itakusaidia kuepuka majumuisho ya kwamba wanafunzi wa darasa hili hawafundishiki kama tulivyozoea kusema.

**MAHUSIANO YA MWALIMU NA MWANAFUNZI**

Sehemu hii tuianze kwa kunukuu baadhi ya kauli maarufu zinazotajwa na watu wanaoona thamani kubwa ya mwalimu.

i. Mwalimu ni kioo,
ii. Mwalimu ni mlezi,
iii. Mwalimu ni kiongozi n.k.

Tumeshindwa kutaja wahusika waliowahi kuwalinganisha walimu na dhana hizo tulizozirejelea kutokana na kauli hizo zinatajwa tu na watu mbalimbali. Je kuna ukweli gani katika hilo? Ukifuatilia katika mataifa yaliyowatupa walimu mbali na kuiona kama kazi iliyodharaulika watakwambia kwamba hizo ni kejeli, kudanganyana, na kupewa sifa ambazo hazipo. Aidha, katika hali halisi ukweli unaonekana. Jiulize kioo ni nini? Kiongozi je? Na mlezi vipi?

Mwalimu pamoja na kufundisha darasani anakwenda mbali zaidi ya hapo. Ujifunzaji darasani ni sehemu tu kwa mwanafunzi, mambo mengi anajifunza nje ya darasa. Masuala mengi ya kijamii na kitamaduni hayafundishwi ndani ya darasa bali nje ya darasa. Jiulize, nani aliyekufundisha kutembea hivyo unavyotembea? Hivyo unavyoandika kwa kuzikunja herufi za maandishi yako ili zionekane zinavyooneka? Namna unavyovaa? Unavyoongea? Na mengine mengi. Je, mambo hayo ulijifunza darasani? Ulizaliwa na aina ya ubunifu ulionao? Kama jibu lako likiwa hapana utakuwa unakubaliana na hoja kwamba mwalimu hatazamwi ndani ya darasa pekee. Rejea mfano ufuatao;

> Baba alitoka kazini mapema akawa amejipumzisha nyumbani mbele ya kiambaza cha mlango anasoma magazeti aliyoyanunua wakati anatoka kazini. Mtoto wake apatae miaka mnne alikuwa anacheza uwanjani na mama yake yupo jikoni kushughulikia masuala ya nyumbani. Mara baba alisikia sauti ya mtoto akiomba msaada kwa baba. Kutazama akamuona mtoto anakuja anakimbia huku akifuatwa na jibwa kubwa limeachama kiasi linatishia uhai wake pia. Baba aliogopa akainuka na kuingia ndani na kufunga mlango. Mtoto nje ya mlango alidondoka akisubiri kudra za Mungu kumuokoa. Bahati nzuri lile jibwa halikumdhuru yule mtoto, lilimnusanusa na kuamua kujiondokea. Simulizi letu.

Baba kwa kawaida ndiye mlinzi na kiongozi katika familia. Maswali yanakuja, je mtoto yule baada ya tukio hilo anajenga hisia gani juu ya baba yake? Je, mtoto siku moja akikanusha kumwita baba kwa jina ‘baba’ kama linavyojulikana atakuwa anakosea? Je, mtoto anaweza kuamini kwamba anausalama wa kutosha dhidi ya hatari yoyote ile anapokuwa nyumbani? Fikiria kwa upande wako ingekuwaje?

Maswali yaliyotangulia na mfano wa simulizi hapo juu ni kielelezo cha majukumu aliyonayo mwalimu. Kwa kawaida watoto wawapo shuleni wanajivunia si taaluma tu wanayopatiwa na walimu wao, bali ulinzi madhubuti. Mwalimu ndiye mzazi (Baba) kwa maana ya mfano hapo juu. Watoto wanajisikia kuwa salama wanapokuwa na walimu wao darasani na nje ya darasa. Hatari yoyote inayojitokeza katika mazingira ya shuleni, hujivunia kuwepo katika mikono salama ya walimu wao. Usalama unaojadiliwa hapa ni hali zote za changamoto ya kimazingira, na kitaaluma.

Changamoto za kimazingira ni kama uhaba wa vifaa vya kuwezesha ujifunzaji, kwa mfano, ukosefu wa madarasa ya kutosha ukilinganisha na idadi ya wanafunzi waliopo, madawati, vitabu, vyoo, na samani nyingine. Mwalimu anadhani hana jukumu lolote katika sababu hizi za uhaba wa vifaa vya kufundishia. Kama hili likiwa hivi mwalimu anaingia katika kundi la baba kumkimbia mwanae aliyekuwa akifukuzwa na mbwa kwa lengo la kumshambulia. Ni jukumu la mwalimu kuifanya hali iliyopo kukabiliana nayo ikiwa ni pamoja na kutoa mbinu mbadala za kutumia vifaa vichache vilivyopo kufanikisha lengo la kujifunza.

Kuhusu changamoto za kitaaluma, mwalimu ndiye kiongozi mkubwa shuleni. Wanafunzi wanamwamini mwalimu kuliko mwanajamii mwingine nje na ndani ya darasa. Hii ni kusema kwamba, mwalimu hatakiwi kutoa majawabu ya matatizo ya kitaaluma ambayo hana uhakika nayo. Kufanya hivyo ni makosa makubwa ambayo yanaweza kuchukua muda mrefu kusuruhishwa. Kwa mfano, mwalimu mmoja aliwahi kunifundisha juu ya mmea wa mkokoa kwamba ni kama

mmea wa karanga. Kutokana na mazingira halisi ya kijiografia niliweka picha ile akilini. Baadaye nilibahatika kwenda katika shughuli za kikazi katika wilaya ya Kyela ambapo mikokoa inalimwa. Jamaa yangu alinionesha mti wa mkokoa nikambishia kwamba yeye alikuwa hajui. Tukio hili lilitokea baada ya miaka takribani kumi (10) lakini taswira ile ya mmea wa mkokoa na mmea wa karanga alionifundisha mwalimu wangu haijanitoka katika fikra zangu. Je nani mwenye tatizo? Mwalimu yawezekana hakuwahi kuuona mkokoa, lakini akakosea kwa kutoa majawabu yasiyo sahihi. Je wanafunzi wengine waliofundishwa hivyo na hawajawai kuuona mmea huo wa mkokoa halisi unaweza kuwaaminishaje? Fikiria hali hiyo na linganisha majukumu aliyonayo mwalimu.

## HITIMISHO

Makala hii imeonesha kuwa Kiswahili kina nafasi muhimu katika kujenga umahiri wa lugha na maarifa kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini Tanzania. Ufanisi wa ujifunzaji hutegemea mwingiliano wa ufundishaji bora, matumizi ya lugha inayofahamika kwa wanafunzi na mazingira rafiki ya shule. Hivyo, kuboresha elimu ya msingi kunahitaji kuimarisha kwa pamoja sera ya lugha, mbinu za ufundishaji na mazingira ya ujifunzaji ili kuhakikisha mwanafunzi anapata maarifa yenye tija kwa maendeleo yake binafsi na ya taifa.

## MAREJELEO

Bruner, J.S (1960). *The Process of Education*. Havard University Press.

Garder, R. (1985) *Social Psychology and Social Language Learning*: The Role of Attitudes and Motivation. London: Edward Anorld.

Madila, Z na Yesaya, S (2025) *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili Sekondari na Vyuo*: Nadharia na Vitendo, Uzingativu wa Mtaala Mpya na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la Mwaka 2023 nchini Tanzania. Simulizi Afrika Publishers. Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B (2016) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Taasisi ya taaluma za Kiswahili (TATAKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Msanjila, Y. P. (2004). *Kiswahili Kitumike Kufundishia Sekondari na Elimu ya juu Tanzania*. Dar es Salaam: TUKI.

Mwanahewa, S (1997). *Misingi ya Ufundishaji wa Kiswahili*: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Onyango, J. O (1990). *Mielekeo ya Wasomi Kuhusu Matumizi ya Kiswahili Nchini Kenya*. Nairobi: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Kenyata.

Richard, J. C and Rodger, T. S (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching*. New York: Cambridge University Press.

Sewangi, S.S. (2004). *Nafasi ya Lugha katika Maendeleo ya Uchumi*: Mfano wa Kiswahili Kiswahili katika Tanzania. Katika Kihore.Y.M na Chuwa A. R (wah). Kiswahili katika Karne ya Ishini na Moja. Dar es Salaam: TUKI.